



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO



Simu Na. 0737 205318
Nukushi: 0 732 951 745
Baruapepe: ded@busokelodc.go.tz
Kumb. Na. BDC/A.2/01/58

Mkurugenzi Mtendaji,
S. L. P. 2,
TUKUYU.
31/05/2023.

YAH: TANGAZO LA NAFASI MOJA (1) YA KAZI YA KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anatangaza nafasi moja (1) ya kazi ya Katibu Mahsus daraja la II baada ya kupata kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi chenye kumb. Na. FA.97/228/01"TEMP"/06 cha tarehe 06/04/2023.

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe na elimu ya kidato cha nne
2. Awe na Astashhada (NTA level 6) ya mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihami wa hatua ya tatu.
3. Awe amefaulu somo la Hati Mkato ya kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) au chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU:

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka mbalimbali.
2. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
3. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
4. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi wake.
5. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maafisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
6. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

MSHAHARA;


Kwa kuzingatia Muundo na Ngazi za mshahara ya watumishi wa Serikali yaani TGS C1 kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA MUOMBAJI.

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yeyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo.
2. Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote yaambatishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) namba za simu na anuani sahihi.

4. Maombi yote ya waombaji yaambatishwe na nakala ya vyeti vya Taaluma, vyeti vya kidato cha (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) za passport size za hivi karibuni na ziandikwe majina kwa nyuma.
5. Testimonials na "Provisional statement of results" hati ya matokeoya kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya uhakiki iambatishwe kwenye maombi.
7. Siku ya usaili kila muombaji afike na vyeti halisi (Original) vya Elimu, Taaluma, kuzaliwa na Kitambulisho.
8. Waombaji waliostaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Uwasilishwaji wa taarifa na sifa za kughushi ni kosa kisheria na wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
10. Maombi yaambatishwe na nakala ya kitambulisho cha **NIDA.**
11. Maombi yote yatumwe kwa njia ya email ya Mkurugenzi Mtendaji ded@busokelodc.go.tz pia kwa watakaoweza kuleta kwa njia ya mkono katika Ofisi za Halmashauri.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 13/06/2023 saa 9:30 Alasiri


MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUSOKELO

Samwel Oberlin
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO**

Nakala;

1. Katibu wa Tume,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S.L.P 2320,
DODOMA.
2. Tovuti ya Halmashauri
www.busokelodc.go.tz
3. Mbao za Matangazo
Halmashauri ya Wilaya
BUSOKELO.

*Barabara ya Tukuyu, S. L. P 2 Tukuyu, Simu +255 758 007 740, Nukushi: 025 2957492,
Barua pepe: ded@busokelodc.go.tz, Tovuti: www.busokelodc.go.tz*